ELIMU

NA JENIFER GILLA,
BRAZZAVILLE

# Mila na desturi ni tiba mpya ya kuhifadhi viumbe, mazingira Afrika

MATUMIZI ya mila na desturi za wananchi wazawa wa sehemu zenye misitu asilia barani Afrika yamedhihirika kuwa ni mkakati unaofaa kutunza bayoanuai zilizopo ndani ya misitu inayowazunguka kwenye kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Ni maelezo ya wanawake wazava wanaosema kuzingatia mila na desturi zao ni njia kuu wanayoitumia kutunza viumbe hai kuanzia wanyama, wadudu, mimea na viumbe wengine kwenye maeneo yao ya Afrika ya Kati na Bonde la Kongo.

Wanayasema hayo kwenye Kongamano la Kwanza la Wanawake Wazawa wa Afrika ya Kati na Bonde la Kongo linalofanyika Brazzaville, nchini Jamhuri ya Congo linaloandaliwa na mashirika ya REPALEAC na Right Resources Initiative (RRI).

Baadhi ya mila hizo ni kukataza kula kila nyama inayopatikana katika misitu yao pia kuingia bila kibali kutoka kwa viongozi wa kimila kwa kuwa inaaminika misitu hiyo hulindwa na mizimu, aidha kuficha aina za miti dawa wanayoitumia kuepusha wageni kuivamia na kuimaliza.

Kadhalika, wanataja mila nyingine ni kuwachukulia wanyama kama ni ndugu na marafiki wao hivyo wanapopita katika maeneo yao hawawagusi pamoja na kufunga shughuli za kuvua na kuchota maji kwenye mito kwa muda huku wakiamini kuwa inalindwa na mizimu.

Mariam Gisero kutoka mkoani Mara, akizungumzia ulinzi wa misitu kwa kutumia mila na desturi zinazohusisha wanawake, anaiambia Nipashe kuwa anatoka kwenye msitu wa Mibango Butiama, akisema wanaamini kuwa msitu huo unalindwa na mizimu ya mababu zao hivyo yeyote haruhusiwi kukata miti bila kibali kutoka kwao.

“Inaaminika kuwa yeyote atakayekwenda kinyume ataiudhi mizimu ambayo hugeuka wanyama wakali na kumdhuru. Imani hiyo imechangia kuhifadhi bioanuai iliyopo katika misitu hiyo.”

Kutoka Kenya, Teresa Chemosop kutoka jamii ya Waogiek, analiambia Kongamano la Kwanza la Wanawake Wazawa wa Afrika kuwa, anapotoka hairuhusiwi kuua tembo kwa sababu anaaminika kuwa ni ndugu wa wanadamu na atakayefanya kosa hilo anaachiwa laana na ukoo ambayo humfanya kuwa kichaa au kupotea hapo kijijini.

“Sisi tembo ni ndugu yetu wa damu, atakayebainika amemuua anapelekwa kwenye baraza na kuonywa na yeye anaapa kuwa hatorudia na ikitokea kuwa amerudia analaaniwa na ukoo na kutoweka ,” anasema.

Kiongozi wa jamii za wazawa kutoka kijiji cha Bananing nchini DRC, Kabile Angel, anasema katika kijiji chake wanawake hawaruhusiwi kula nyama ya chui kwa kuwa inaaminika atakayekula anaaibisha mila hivyo atapata madhara ikiwamo kuugua.

Anasema pia si kila mwanamke anaruhusiwa kwenda kuchimba dawa msituni, bali kuna watu maalum wenye utaalamu wa namna ya kuchuma dawa hizo na hiyo inafanyika ili kuepuka uharibifu wa miti inayotoa dawa hizo na taarifa zake kufahamika kwa jamii za nje na mbali ambazo zinaweza kuiharibu.

“Kuna namna maalum ya kuchuma dawa, kwa sababu kuna miti ukiikata vibaya inakufa, kwa hiyo kuna watu wenye utaalam na kuzijua dawa hizo kikamilifu ndiyo wanaokwenda kuchuma, yoyote atakayekwenda kinyume na masharti haya anaadhibiwa,” anasema.

Naye Ndumeimana Gracia kutoka Burundi, anaeleza kuwa katika jamii yake huwa wanafunga mto kwa muda kuwa hakuna mwanamke anayeruhusiwa kuchota maji au kuvua samaki katika kipindi hicho na atakayekiuka kama hataombewa msamaha kwa mizimu atapata madhara.

Mkurugenzi wa Mikakati wa Shirika la kiraia la Christensen Fund la Marekani, Casey Box , linalotoa msaada wa kifedha kwa wazawa ili kulinda rasilimali zao anasema mila na desturi zina nafasi kubwa ya kuhifadhi mazingira kwa wazawa wa jamii zenye misitu barani Afrika.

Anaeleza kuwa mfuko wa Christensen Fund, unawekeza kuimarisha uhusiano kati ya mazingira asilia na tamaduni za wanadamu na kwamba hutoa ruzuku zinazokuza manufaa ya ulinzi jumuishi wa kibaolojia, kiikolojia na kitamaduni katika maeneo mbalimbali duniani ikiwamo Congo.

Anasema kwa uzoefu aliokuwa nao wa kufanyakazi na wazawa wa jamii zilizozungukwa na misitu kwa miaka 10 amegundua licha ya juhudi kubwa wanazofanya wazawa ya kuhifadhi bioanuai wana changamoto ya kutokuwa na usalama wa maisha yao baada ya kuibuka tabia ya serikali kuwaondoa kwenye maeneo yao.

“Nafikiri hakuna haja ya kuwaondoa wazawa hawa, serikali inapaswa ikae nao chini kuangalia njia bora wanaweza kufanya ili waendelee kuwapo bila kuathiri shughuli ya uhifadhi, hili jambo linawezekana kwa sababu tumeona baadhi ya maeneo jamii zinaishi na wanyamapori bila tatizo lolote,” alisema.

Mratibu kutoka Shirika la RRI la Marekani, Solange Bandiaky-Badji, anazishauri serikali kushirikiana na jamii hizo ili ziendelee kutunza rasilimali kupitia imani zao ili jamii nzima ikiwamo taifa inufaike na uwapo wake.

“Shirika letu limekuwa likisaidia wanawake wazawa walioko katika jamii zilizozungukwa na misitu kwa sababu tunaelewa nguvu waliokuwa nayo katika kuzihifadhi, lengo ni kuhakikisha wanaendelea kutumia mila na desturi zao kulinda na kuhifadhi rasilimali hizo muhimu,” anasema.




Jamii za watu asilia wataalamu wa fani mbalimbali za jadi wakishiriki kongamano jijini Brazzaville. **PICHA: JENIFFER GILLA**

## Msondo kufunza watoto, mabinti unyumba anguko la elimu

**INATOKA UK.11**

ambao wapo shule za msingi na sekondari kutumia mafunzo hayo kuanza mahusiano tena na wavualana wanaosoma nao, hawajali kuhudhuria masomo, hawafanyi vizuri darasani, kuacha shule bila kuulizwa na wazazi, walezi au wanajamii.

Mbaya zaidi huamua kubaki wengine huolewa mapema huku wakikatisha ndoto zao za kielimu. Anakumbusha kuwa wengi wao ni watoto ambao wana chini ya miaka 14 , miili na akili zao bado hazijawa imara na kuwa na uwezo wa kuhimili maisha ya ndoa. Hivyo suala hili linawafanya baadhi ya wanajamii hao ambao walitakiwa kuwa wanafunzi katika shule mbalimbali kushindwa kufikia ndoto zao za kielimu na kupata madhara ya kiafya pia.

**MADHARA KWA WASICHANA**

Kulingana na maelezo ya msimamizi wa mradi Edna, ni pamoja na watoto wa kike kujifunza zaidi mambo ambayo si muhimu katika maisha yao kwa sasa. Mfano mtoto wa kike wa miaka sita au nane kujifunza jinsi ya kuishi na mwanaume wakati hajapevuka hupelekea kufikiria mambo ya mapenzi na wanaume kuliko masomo.

Na mwisho hufanya watoto kuanza kuona kuwa elimu si kitu cha msingi sana katika maisha yao bali mahusiano ya kimapenzi na kuishi na wanaume ni kipaumbele. Mbaya zaidi hali hii huanza kuathiri maendeleo yao ya kielimu, kiafya, jamii, uchumi na maendeleo ya vijiji vyao.

Anatoa mfano kuwa baada ya mafunzo ya msondo wanafunzi wengi wa kike wamekuwa wakianza kujihusisha na masuala ya mapenzi na watoto wenzao shuleni, mitaani, walimu na pia wanajamii wengine japo bado shuleni.

Wengine wanaamua kuacha shule, kuolewa wakiwa katika umri mdogo tena bila kuwa na ujuzi wala stadi za maisha na uwezo wa kujitegemea kijamii na kiuchumi.

**UFUMBUZI**

Edna anasema kwanza jamii lazima itambue kuwa mafunzo ya msondo kwa watoto si jambo mbaya ila wajali umri na mahitaji yao ya muda mfano kama ni kusoma waachwe wamalize shule, pili, matumizi na mafunzo sahihi ya msondo inatakiwa iangaliwe vizuri na isitumike vibaya ili kuwafanya watoto wa kike kuanza kujifunza mambo ya ndoa na jinsi ya kuishi na mwanaume.